

## 2 : TAUHEED AL-ULUHIYYAH.

Maana yake ni kumpwekesha Allah (sw) katika aina zote za Ibada, kwamba asifanye mwanadamu na kuabudu pamoja na Allah (sw) kiumbe yejote na kujikurubisha kwake huyo kiumbe.

Tauheed hii ndio tauheed muhimu sana kuifahamu, ndio tauheed ambayo Allah (sw) kawaumbia viumbe wote kwa ajili yake Allah (sw).

قال تعالى: ﴿وَمَا خَلَقْتُ الْجِنَّةِ وَالْإِنْسَانَ إِلَّا لِيَعْبُدُونِ﴾ [الذاريات: ٥٦]

Allah (sw) anasema: ("Sikuwaumba majini na binadamu isipokuwa ni kwa lengo la kuniabudu") (Adhariyat: 56).

Tauheed hii ndio ambayo Allah (sw) aliwatuma mitume wake, akawateremshia na vitabu.

قال تعالى: ﴿وَمَا أَرْسَلْنَا مِنْ قَبْلِكَ مِنْ رَسُولٍ إِلَّا نُوحِيَ إِلَيْهِ أَنَّهُ لَا إِلَهَ إِلَّا هُوَ فَاعْبُدُونِ﴾ [الأنبياء: ٢٥].

Allah (sw) anasema: ("Hatukutuma Mtume wa aina yoyote kabla yako isipokuwa tulimfunulia ya kuwa hapana mola aabudiwaye kwa haki isipokuwa mimi (Allah) basi niabuduni") (Al-anbiyah: 25).

Tauheed hii ndio ambayo washirikina waliikataa na kuipinga wakati walipolinganiwa na mitume wa Allah (sw).

قال تعالى: ﴿قَالُوا أَجِئْنَا لِنَعْبُدَ اللَّهَ وَحْدَهُ وَنَذَرَ مَا كَانَ يَعْبُدُ آبَاؤُنَا﴾ [الأعراف: ٧٠]

Allah (sw) anasema ("Wakasema kumwambia Hud, je umetuita tumuabudu mwenyezi mungu peke yake, na tuihame ibada ya masanamu ambayo tuliiirthi kutoka kwa baba zetu") (Al-A'raf: 70).

Haifai kufanya aina yoyote ya ibada kwa asiekuwa Allah (sw), sio kwa Malaika aliye karibu na Allah (sw), wala Nabii aliyetumwa, wala kwa Walii aliye kuwa mwema, wala yoyoye katika vumbe vyake Allah (sw), kwani haifai ibada ya aina yoyote kufanya wa asipokuwa ifanywe kwa ajili ya Allah (sw).